muhimu cha utoaji wa mafunzo na elimu ya viwango vya juu katika fani mbalimbali.

Dk Mwinyi alisema hayo alipokutana na wajumbe wa Tume ya Utumishi ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wakiongozwa na Spika wa

kwa taifa.

Dk Mwinyi alisema uwepo wa chuo hicho utachochea ujio wa wanafunzi na wataalamu kutoka mataifa mbalimbali kwenda kujifunza Zanzibar.

Alisema Serikali ya Zanzibar ipo

liko ya maendeleo Zanzibar, hususani katika ujenzi wa miundombinu ya barabara na kasi ya ukuaji wa uchumi inayoendana na mabadiliko ya dunia.

Awali, Dk Mwinyi alisema serikali imejipanga kumaliza tatizo la usafiri na usafirishaji wa mizigo katika Kisiwa

# Serikali yadhamiria matumizi mifumo ya kidijiti salama

Na Selemani Nzaro, Arusha

MAMLAKA ya Serikali Mtandao (eGA) imesema serikali imedhamiria kutumia mifumo ya kidijiti iliyo salama na jumuishi ili kuongeza ufanisi, tija, uwazi na uwajibikaji katika utendaji kazi na kuboresha huduma zinazotolewa kwa wananchi.

Mkurugenzi Mkuu wa eGA, Benedict Ndomba alisema hayo Arusha kwenye ufunguzi wa kikaokazi cha Sita cha Serikali Mtandao jijini Arusha juzi.

Ndomba alisema eGA imeendelea kutekeleza jukumu lake la msingi la kuratibu, kusimamia na kukuza jitihada za serikali mtandao kwa kuhakikisha matumizi ya Tehama serikalini yanakuwa salama na shirikishi na kuzingatia viwango na miongozo ya Serikali Mtandao.

Alisema mamlaka hiyo imeimarisha usimamizi wa miradi ya Tehama serikalini, usimamizi na uendeshaji wa Mtandao wa Mawasiliano Serikalini (GOVNET) pamoja na uoni wa jumla wa mifumo ya Tehama ya serikali na mingine inayotoa huduma serikalini.

Ndomba alisema hali hiyo imechangia kupunguza urudufu wa mifumo, kuimarisha ubadilishanaji wa taarifa serikalini baina ya mifumo ya taasisi mbalimbali pamoja na kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za umma kwa kutumia Tehama.

"Hii ni sehemu ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2050 kupitia lengo la kuhakikisha, zaidi ya asilimia 80 ya huduma za serikali zinapatikana kupitia mifumo ya kidijitali iliyo salama na jumuishi ifikapo mwaka 2050. Pia ni utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2025 Ibara ya 46 ambayo pamoja na mambo mengine inaelekeza huduma za serikali asilimia 50 zipatikane kupitia mifumo ya kidijiti ifikapo 2030," alisema Ndomba.

Aidha, alisema mamlaka imeendelea kuimarisha usimamizi na uendeshaji wa Vituo Vya Serikali Vya Kuhifadhi data ambavyo vimewezesha taasisi nyingi za serikali kuhifadhi na kuendesha mifumo yao kwa usalama, ufanisi na uhakika wa upatikanaji wa huduma kwa wakati wote. Hatua hii imeongeza usalama wa taarifa za serikali na kupunguza gharama za uendeshaji wa miundombinu ya Tehama.

Vilevile aliongeza kuwa mamlaka imefanikiwa kuimarisha uwezo wa taasisi za umma kutekeleza jitihada za serikali mtandao kupitia mafunzo, usimamizi na ushauri wa kitaalamu, jambo ambalo limeongeza ufanisi katika usimamizi na uendeshaji wa miradi ya Tehama katika taasisi za umma. Kwa upande wake Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA), Dk Mussa Kissaka alisema kikao hicho kinawakutanisha viongozi wa taasisi za umma, wataalamu wa Tehama, sekta binafsi na wadau wengine wa serikali mtandao kwa lengo la kubadilishana uzoefu, kujadili mafanikio na changamoto na kuweka mikakati ya pamoja ya utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Miongozo na Viwango vya Serikali Mtandao.

Alisema mafanikio ya ajenda hiyo yanahitaji mshikamano na ushirikiano wa karibu wa wadau wote, kuanzia hatua za upangaji hadi utekelezaji na ufuatiliaji wa miradi ya Tehama katika taasisi zote za umma.

Naye Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Ikulu, Mululi Mahendeka alisema serikali mtandao imeendelea kuwa nyenzo muhimu kuimarisha utawala bora na ufanisi katika utendaji kazi na utoaji wa huduma kwa wananchi katika kipindi hiki cha mabadiliko ya kasi ya teknolojia.



Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Dk Batilda Burian ak
mwanamuziki nguli wa dansi, Steven Hizza kwe
Tanga jana. Hizza alifariki dunia juzi akiwa nyu
humo. (Na Mpigapicha Wetu).

# CCM yataka serikali k wa wakulima na wafu

Na Shakila Mtambo Urambo

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimemuagiza Mkuu wa Wilaya ya Urambo mkoani Tabora, Dk Hamis Mkanachi aingilie kati mgogoro wa wakulima na wafugaji.

Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM Itikadi, Uenezi na Mafunzo, Kenani Kihongosi alitoa maelekezo hayo wakati wa mkutano wa hadhara alipokutana na wananchi kusikiliza na kutatua kero zao uliofanyika Urambo juzi.

Kihongosi aliagiza hivyo kutokana na malalamiko ya wananchi juu ya baadhi ya wafugaji kuingiza mifugo yao katika mashamba ya wakulima na kuwasababishia hasara ya uharibifu wa mazao ya wakulima hao.

"Hakuna aliyejuu ya sheria iwe mfugaji iwe mkulima na kumekuwa na changamoto hii kwa wafugaji kuingiza mifugo yao kwa wakulima na ikitokea wakaulizwa wanachukua fimbo

wanaanza kuwachapa
jambo namuomba mku
wilaya akakutane na w
na wafugaji na afanye
na atoe onyo litakaloke
matendo haya," alisem

Alisema ni muhim
kusimamia sheria na
hatua ili kukomesha
hivyo kutokana na ba
wafugaji kusababisha
wa mazao na kutishi
na maisha ya watu n
lazima isimamie mi
ili kila mwananchi a
yake.

Kihongosi aliser
serikali duniani ina
kumkandamiza m
wake hivyo dhami
ya Awamu ya Sita
sha maendeleo ya
wananchi wote hu
moto zikitatuliwa
umzo na busara.

Akizungumzi
ya wafanyabiash
la ndizi waliohar
uongozi wa wila
fanyabiashara h
wasiwasi wao k